

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Kufukuzwa kwa Odiljon Jalilov Kunahatarisha Maisha Yake

(Imetafsiriwa)

Jioni ya mnamo Oktoba 29, Odiljon Jalilov, mwanachama wa Hizb ut Tahrir/Sweden, alipatikana na polisi na kuwekwa chini ya ulinzi akisubiri maandalizi ya kuhamishwa hadi Uzbekistan.

Uzbekistan ina historia ndefu na inayojulikana ya ukandamizaji dhidi ya wapinzani wa kisiasa, hata mbaya zaidi dhidi ya wapinzani wa Kiislamu, wanachama wa Hizb ut Tahrir. Wanachama wetu wameteseka kwa miongo mingi kutokana na vifungo virefu vya jela, mateso na hata mauaji nchini Uzbekistan. Vyanzo kutoka kwa familia ya Odiljon Jalilov nchini Uzbekistan vinasema polisi wamekuwa wakiwasiliana na familia yake na wamewafahamisha kuwa Odiljon Jalilov ataregeea hivi karibuni. Kufukuzwa na kukabidhiwa kwa mwanachama wetu, Odiljon Jalilov, kwa serikali dhalimu ya Uzbekistan kunawakilisha tishio la kihakika kwa maisha yake ambayo mamlaka za Uswidi zitawajibika kwayo endapo uhamishaji huo utafanywa.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir
Uswidi**